

**HOTUBA YA MHE. NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO MHANDISI ATASHASTA NDITIYE KATIKA UZINDUZI WA WIKI YA SHIRIKA LA RELI TANZANIAPAMOJA NA KUZINDUA NEMBO MPYA YA TRC**

**Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi Dkt. Leornard Chamuriho,**

**Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi TRC Profesa John Wajanga Kondoro,**

**Muwakilishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali,**

**Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Bandari- Mhandisi Deusdedit Kakoko,**

**Mkurugenzi Mkuu SUMATRA- Gilliard Ngwewe,**

**Wawakilishi wa wadau wa TRC :-**

- **Kampuni ya Bakhresa**
- **WFP**
- **Kampuni ya YARA**
- **Wawakilishi wa vyama vya wafanyakazi TRAWU na TAMICO**
- **Uongozi wa TRC**
- **Wafanyakazi wa TRC**

**Wageni waalikwa, waandishi wa habari mabibi na mabwana**

## **Habari za asubuhi**

Awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia Afya njema na kutuwezesha kukutana katika Hafla hii ya kihistoria kwa Shirika letu la Reli, watazania wote na dunia kwa ujumla.

Shirika letu la Reli kwa sasa linapitia katika mageuzi makubwa yanayolenga kulifanya Taifa letu kuingia kwenye uchumi wa kati (wa viwanda) katika kipindi cha miaka michache ijayo.

## **Wageni waalikwa Mabibi na Mabwana**

Uongozi wa Shirika la Reli Tanzania limeandaa wiki ya TRC kwa lengo la kuwapatia fursa watazania kufahamu kwa kina majukumu ya Shirika la Reli Tanzania, huduma zitolewazo yaani huduma ya usafirishaji wa abiria na mizigo pamoja na kufahamu miradi mikubwa miwili inayosimamiwa na TRC, yaani mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa –SGR na mradi wa uboreshaji wa reli ya kati (Dar-Isaka) pamoja na miradi mingine kama kufufua njia za reli ya zamani (Tanga, Arusha na Moshi) ujenzi wa Reli ya Mtwara – Mbambabay kupitia Liganga na Mchuchuma ipo kwenye hatua za awali za kumpata Mshauri Mwelekezi wa fedha baada ya hatua zote za awali kukamilika.

## **Wageni waalikwa Mabibi na Mabwana**

Juhudi hizi zinazofanywa na serikali ya awamu ya tano kupitia Ilani ya CCM katika sekta ya usafirishaji zitapelekea kuondoa kero mbalimbali na kukuza vipato vya wananchi ili kuhakikisha kauli mbiu ya Uchumi wa viwanda inatekelezwa kwa ufasaha kwa kutumia miundombinu ya reli ya kisasa na uboreshaji wa reli ya kati Dar- Isaka. Mara baada ya reli hizi kukamilika, kwa upande wa reli ya kisasa itakua na uwezo wa kubeba mizigo/abiria zenye uzito mkubwa mpaka tani 10,000 kwa treni moja, mwendo kasi wa kilomita 120 kwa saa kwa treni za mizigo, na treni za abiria kwa mwendokasi wa kilomita 160 kwa saa, Aidha itaokoa muda kwa wadau watakaotumia Huduma za Shirika la Reli hasa wafanyabiashara wakubwa na wadogo.

## **Wageni waalikwa Mabibi na Mabwana**

Kupitia miradi hii inayosimamiwa na TRC Watanzania wanapata fursa za ajira, kujiongezea kipato na kuwajengea ujuzi wale wote wanaoshiriki katika shughuli za mradi kwa kuwa watapata fursa yakujifunza kwa vitendo ujuzi mpya unaoletwa na wakandarasi wa kigeni nchini.

Ili kuhakikisha reli hizi zinafanya kazi kwa ufasaha na kujiendesha kifaida Shirika la Reli Tanzania kwa sasa linaendelea kutoa mafunzo ya awali ndani ya nchi kuhusu huduma za usafirishaji kwa njia ya reli, ukarabati wa miundombinu ya reli na miradi inayosimamiwa na kuratibiwa na TRC kwa

vijana 160 wa kitanzania na baadae baadhi watapelekwa Nchi za nje kama Ethiopia, Korea, China na Ujerumani. Lengo ni kuhakikisha kuwa mara baada ya miradi hii kukamilika Shirika linaweza kujiendesha kwa ufanisi ulio bora zaidi na kuliingizia taifa kipato kwa maendeleo endelevu ya nchi.

### **Wageni waalikwa Mabibi na Mabwana**

Leo tunazindua rasmi nembo ya TRC pamoja na kanuni 10 za reli tayari kwa utekelezaji wa Sheria Namba 10 ya Reli ya mwaka 2017, na kwa uzinduzi huu Shirika la Reli Tanzania sasa linasimama kwa sura mpya ya kibiashara, ufanisi na kutoa huduma bora na za kuaminika kwa wadau mbalimbali nchini. Reli ya kisasa inajengwa kwa awamu. Awamu ya kwanza ina urefu wa kilomita 1,219, bila kujumuisha njia za kupishana na imegawanywa sehemu tano (5).

Kwanza: Dares Salaam- Morogoro km 300, pili: Morogoro - Makutupora km 422, tatu: Makutupora -Tabora km 367.25, nne: Tabora - Isaka Km 167.5 na tano: Isaka-Mwanza Km 311.4.

### **Wageni waalikwa Mabibi na Mabwana**

Kutokana na juhudi zinazofanywa na serikali ya awamu ya tano nawahamasisha wananchi wa Tanzania tushirikiane kwa pamoja kuunga mkono juhudi za Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Dr. John Joseph Pombe Magufuli katika utekelezaji wa mipango iliyopangwa kwa

manufaa ya watanzania na kila mmoja wetu awe mlinzi wa miundombinu ya reli kwa kuwa Reli hizi ni mali ya watanzania.

Aidha, nichukue fursa hii kuwapongeza wafanyakazi wa Shirika la Reli Tanzania kwa kutekeleza wajibu wenu ipasavyo kwa kuratibu na kusimamia vema shughuli za miradi, niwahakikishie kuwa serikali ya Awamu ya tano itaendelea kuboresha huduma kwa wananchi na kuimarisha miundombinu ya reli kwa manufaa ya maendeleo ya Taifa letu.

Baada ya maneno haya machache sasa napenda kutamka kuwa nipo tayari kuzindua rasmi nembo ya TRC pamoja na kanuni 10 za reli tayari kwa utelezaji wa Sheria Namba 10 ya Reli ya mwaka 2017, kwa maendeleo ya Shirika letu, Taifa na wananchi kwa ujumla.

**Asanteni kwa kunisikiliza.**